# Ufalme wa Mbinguni na Torati

Imeandikwa na Respicius K. Luciani

https://www.sayuni.co.tz

Ndugu yangu Mkristo, kila siku unasali, “Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama [yanavyotimizwa] mbinguni …” Na unamalizia, “Kwani ufalme ni wako, uweza na utukufu hata milele yote. Amina!

Sasa ndugu yangu Mkristo, unaweza kuniambia ufalme wa Mungu unaoomba uje una hulka gani? Unayajua mapenzi ya Mungu unayoomba yafanyike? Umeshawahi kutafakari juu ya masuala haya? Umeshawahi hata *kuanza* kufanya utafiti katika Biblia, unaoongozwa na Roho Mtakatifu, ili upate kuyajua mapenzi ya Mungu? Huko mbinguni mapenzi ya Mungu yanatimizwaje? Muhimu zaidi, ufalme wa Mungu unaouomba utaendeshwa kwa kanuni na sheria gani?

Kwa hakika, mapenzi ya Mungu yanatimizwa kwa utimilifu huko mbinguni; wewe unaomba yatimizwe vivyo hivyo hapa duniani. Je, unajua maana yake kwako?

Kama majibu yako ya maswali haya ni ‘hapana!’ basi sala yako hii inahitaji kuboreshwa na ufahamu kutoka katika Biblia ili *angalau uanze* kutimiza mapenzi ya Mungu hapa duniani. Ndiyo, tunaomba ‘mapenzi yako yatimizwe’, lakini wengi wetu hatujui kwamba anayepaswa kutimiza mapenzi hayo ni sisi wenyewe!

“Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkafundishe mataifa yote, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu: Mkiwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi: na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata mwisho wa ulimwengu. Amina.” Hayo ni maneno ya Bwana Yesu kwa wafuasi Wake; kwa kifupi, ufalme tunaoomba uje, umeshakuja. “… ikiwa ninafukuza pepo kwa kidole cha Mungu, bila shaka ufalme wa Mungu umewajia.” Luka 11:20. Shika kwa makini maneno hayo, ‘… ninafukuza pepo kwa kidole cha Mungu …’ Kwa hakika tunajua kwamba Yesu alifukuza pepo. Wanafunzi Wake walifukuza pepo – Matt. 12:27; Mar. 16:17; Luke 10:17. Uinjilisti, mafundisho sahihi ya neno la Mungu, matendo mema / kushika amri za Mungu, utawala wa Kikristo katika taasisi, miji, vijiji, nchi mbalimbali, nk; hizo ni chache tu kati ya dalili za uwepo wa ufalme wa Mungu hapa duniani. Lakini, uovu, udhalimu, upo pia, tena kwa kiasi kukubwa sana.

Maana yake ni kwamba ufalme huu [wa Mungu] unapaswa kupiganiwa. Kwani katika utawala huu, sisi Wakristo tunatawala Naye; na Yeye ndiye Mtawala Mkuu. Soma War. 8:17; 2Tim. 2:12; Ufu. 3:21; 5:10; 20:6.

Soma Mika 4:1-5; Isaya 2:2-5. Hapo utaiona ile taswira anayotuonyesha Mungu ya jinsi ufalme Wake utakavyokuwa kabla ya ujio wa Pili wa Bwana Yesu. Katika Mika 4:2, tunasoma, “***Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, <u>twende juu mlimani kwa Bwana</u>, na nyumbani kwa Mungu wa Yakobo; <u>naye atatufundisha</u> <u>njia zake</u>, nasi tutakwenda katika mapito yake; kwa maana katika Sayuni itatoka <u>sheria</u>, na neno la Bwana litatoka Yerusalemu***”. Dunia itaenea Ukristo; na wewe Mkristo ndiye utakayefanikisha hili, kwa uweza wa Mungu. Ufalme huu ni lile jiwe aliloliona nabii Danieli katika maono yanayosimuliwa katika Danieli 2:44-45 ya ndoto ya mfalme Nebukadnezza wa Babeli. Katika Kanuni ya Imani tunasema, “Nao ufalme wake hautakuwa na mwisho”. Ufalme huo ndio huu. Sheria ya Mungu, inayoitwa Torati, ndiyo ufunguo wake. Soma Biblia!

Morogoro, +255 679 90 0814, +255 754 37 5474.